Mwongozo wa Jamii kwa Mkakati wa Mfuko wa Kimataifa 2017-2022

eannaso

Regional Platform
for Communication and Coordination
on HIV/AIDS, Tuberculosis and Malaria
For Anglophone Africa

MKAKATI WA MFUKO WA KIMATAIFA UNAHUSU NINI HASWA?

Mkakati wa Mfuko wa Kimataifa kwa kipindi cha 2017-2022 unaitwa “Kuekeza kumaliza Majanga:. Mkakati ni andiko ambalo linaainisha ajenda ya miaka sita. Inatokana na maono, dira na mikakati minne (kila moja na malengo elekezi) ikisaidiwa na viwezeshi viwili vikuu.

MAONO:

Dunia iliyo huru na mzigo wa UKIMWI, Kifua Kikuu na malaria na afya bora kwa wote

DIRA:

Kuvutia, kujiinua na kuekeza rasilimali za ziada kumaliza majanga ya UKIMWI, Kifua Kikuu na malaria na kusaidia kufikia Malengo Endelevu ya Maendeleo.

MALENGO:

Malengo na dhamira za afya za Mfuko wa Kimataifa zimeunganishwa wazi wazi na Mipango ya Washirika wa Dunia (Partners’ Global Plans) (Tizama Kisanduku cha 1).

Maelezo ya Jumla ya Mkakati wa Mfuko wa Kimataifa kwajili ya 2017-2022

KUEKEZA KUMALIZA MAJANGA



Viwezeshi vikuu

Ubunifu na kutofautisha kupitia uendelezi wa kimaendeleo

Kusaidia ubia wa pamoja

MUHIMU KWETU!

Mkakati mpya wa Mfuko wa Kimataifa wa 2017-20122 unaweka msisitizo zaidi katika kuimarisha mifumo ya kiafya, na kukuza haki za binadamu na usawa wa kijinsia.

KISANDUKU 1: MKAKATI MPYA WA MFUKO WA KIMATAIFA UNAJARIBU KUFANYA NINI?

Malengo na dhamira za afya za Mfuko wa Kimataifa zimeunganishwa wazi wazi na Mipango ya Washirika wa Dunia (Partners’ Global Plans) Haya hapa ni baadhi ya dhamira ambazo zinatuhusu sana:

UKIMWI

- Ifikapo 2020, chini ya maambukizi mapya 500,000, chini ya vifo-vitokanavyo na maradhi ya Ukimwi 500,000 na kuangamiza ubaguzi utokao na Ukimwi
- Ifikapo 2020, asilimia 90& ya watu maalum – ikiwa ni pamoja na wauza ngono, wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume, watu wanojidunga sindano, watu waliobadilisha jinsia, wafungwa na wakimbizi – wanapata huduma za kuzuia maambukizi ya Ukimwi.
- Ifikapo 2020, asilimia 90% ya wanawake na wasichana wanaishi bila ubaguzi wa kijinsia na ukatili wa kijinsia ili kuzuia hatari na athari za Ukimwi.

KIFUA KIKUU

- Ifikapo 2020, asilimia 20% na 35% ya visa na vifo vya Kifua Kikuu mtawalia, ukilinganisha na 2015.
- Ifikapo 2025, angalau asilimia 90% ya watu maalum inafikiwa

MALARIA

- Ifikapo 2020, angalau kuwe na upungufu wa idadi ya vifo vya malaria kwa asilimia 40% ukilinganisha na 2015.
- Kuangamiza malaria kwa angalau nchi 10 ifikapo 2020, na angalau ncho 20 ifikapo 2025.

TUCHAMBUE MALENGO MKAKATI MINNE KWA UNDANI!

LENGO #1: ZIDISHA ATHARI DHIDI YA UKIMWI, KIFUA KIKUU NA MALARIA

MALENGO ELEKEZI KATIKA MKAKATI	INA MAANA GANI KWETU
Kuongeza mikakati ya uwazi ambayo inalenga nchi ambazo zina mzigo mkubwa na zilizo na uwezo mdogo wa kiuchumi pamoja na kwa watu maalum na walioathirika na magonjwa hayo matatu	Hii inamaanisha kwamba rasilimali zaidi zitapelekwa kwa nchi maskini zaidi ambazo zimeathirika na magonjwa haya matatu, nyingi ambazo ni za Afrika. Inamaanisha pia kipaumbele kitakua kwa mipango ambayo itaongeza eneo la huduma miongoni mwa watu kama wauza ngono, wanaume wanfanya mapenzi na wanaume, waliobadilisha jinsia, watu wanaotumia dawa za kulevya, wahamiaji, wakimbizi, wafanyakazi wa migodi, wafungwa, wanawake wadogo na wasichana, na watu wengine maalum na walioathirika.
Kuchochea mfumo wa ugawaji na michakato ya athari kubwa, ikiwa ni pamoja na mbinu bunifu tofauti kulingana na mahitaji ya nchi	Hii inamaanisha kwamba lazima pawe na urahisi kwa nchi zinapoomba misaada, ikiachia Mfuko wa Kimataifa kuzingatia mahitaji maalum na muhimu kwako, na kwa nchi yake na kwa kila muktadha husika.
Kusaidia mipango bora ya utekelezaji wa misaasa ikizingatia athari, ubora, uchambuzi wa hatari na thamani ya fedha	Hii inamaana kwamba lazima tuhakikishe hatuharibu fedha za msaada na lazima tuangalie athari za mipango yetu kwa umakini, ili tuweze kuonyesha mafanikio.
Kuimarisha uboreshaji katika kuhoji mazingira magumu ya kiundeshaji kupitia ubunifu na kuongeza urahisi katika ubia	Hii inamaanisha kwamba dhamira ya Mpango wa Kimataifa wa kuhakikisha ufadhili wa Ukimwi, TB na malaria unafikia watu hata katika nchi ambazo zinakumbwa na vurugu za kisiasa, maafa ya asili ama ubovu wa miondomsingi yao kiafya.
Kusaidia mipango endelevu ya kuzuia majanga pamoja na mipito salama	Hii inamaanisha kwamba tunahitaji kufikiria kuhusu na kupanga jinsi mipango endelevu inayosimamiwa na Mfuko wa Kimataifa ipo. Nini kitatokea endapo nchi yako haiwezi kupata fedha za Mfuko wa Kimataifa? Ni mipango gani itaendela? Mfuko wa Kimataifa utatoa usaidizi kwetu kuanza kufikiria kuhusu masuala haya.

LENGO #2: KUJENGA MIFUMO KAKAMAVU NA ENDELEVU YA KIAFYA

MALENGO ELEKEZI KATIKA MKAKATI	INA MAANA GANI KWETU
Kuimairisha mwitikio wa kijamii na mifumo	Hii ni muhimu sana kwetu! Inamaanisha Mfuko wa Kimataifa una dhamira ya kusaidia kazi zetu kama mashirika ya kiraia na makundi ya kijamii kama kipengele muhimu cha mwitikio mzima wa afya.
Kusaidia afya ya uzazi kwa wanawake, watoto na vijana, na misingi ya utoaji wa afya kwa jumla	Hii inamaanisha kwamba mipango yetu ya Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria lazima ijumuishe afya na haki ya uzazi, hususan kwa wanawake na vijana.
Kuimarisha mifumo ya kimataifa na ya ndani ya ununuzi na usambazaji	Upatikanaji wa dawa na bidhaa ni muhimu sana. Tunaweza kuchangia katika ununuzi na usambazaji kwa kuweka mfumo wa uangalizi wa jamii ili kuimarisha ukusanyaji wa takwimu na kuhakikisha usamba-zaji mzuri.
Kuongeza juhudi katika uwekezaji muhimu wa rasilimali watu na afya	Watu wanaotoa huduma za kiafya ni wa muhimu! Hii inajumuisha wafanyakazi wa afya wa kijamii pamoja na wafanyakazi wengine na wanaojitolea ambao wanatoa huduma katika ngazi ya kijamii.
Kuimarisha mifumo ya takwimu ya afya na uwezo wan chi kuchanganua na kutumia	Tunaweza kuchangia takwimu muhimu kuhusu afya na upatikanaji wa huduma kwa kufanya utafiti wa kijamii, kufuatilia na kutoa ripoti mbadala za vielelezo vya jamii.
Kuimarisha na kushirikisha mipango thabiti ya kitaifa ya mikakati ya kiafya na mipango maalum ya kitaifa ya magonjwa	Mfuko wa Kimataifa unataka kufadhili vipaumbele vya nchi. Hii inamaansiha kwamba tunapaswa kuhakikisha vipaumbele vyetu kama mashirika ya kiraia na makundi ya kijamii inajumuishwa katika mipnago ya kitaifa!
Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa kifedha	Tunajukumu la kuhakikisha usimamizi sahihi wa fedha za Mfuko wa Jamii. Tunaweza kufanya ufualiliaji wa bajeti na kuhakikisha tunapata taarifa zilizoko katika akaunti za afya za kitaifa.

LENGO #3: KUKUZA NA KULINDA HAKI ZA BINADAMU NA USAWA WA KIJINSIA

MALENGO ELEKEZI KATIKA MKAKATI	INA MAANA GANI KWETU
Kuongeza mipango ilikusaidia wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na mipango ya kuendeleza afya na haki ya uzazi	Wanawake na wasichana ni nguzo ya mkakati wa Mfuko wa Kimataifa. Hii inamaanisha kwamba wanapswa kuzingatiwa katika kazi zetu za ngazi kitaifa.
Kuwekeza kupunguza ubaguzi katika afya ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa kijinsia na kiumri	Hii inamaanisha mipango inapasa kulenga kupunguza mzigo kwa vijana, wanawake na hususan wanawake wadogo wanakumbwa nayo kutokana na ukaribu wao na magonjwa haya matatu.
Kuanzisha na kuongeza mipango/miradi inayoondoa vipingamizi vya haki za binadamu katika kupata huduma za Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria	Hii inaamisha tunapswa kuweka miradi mahsusi ambayo itapunguza unyanyapaa na ubaguaji, kubadilisha na kuondoa sheria na kanuni ambazo zinazuia na kutenga makundi Fulani, na kuhakikisha usawa wa kijinsia, kukubali bila kushurutishwa na usiri.
Kusaidia katika ushirikishaji wa watu maalum na walioathirika na mitandao katika michakato ya Mfuko wa Kimataifa	Hii inamaanisha lazima tushirikishe Mpango wa Kitaifa wa kimaendeleo pamoja na kufuatilia misaada, ukusanyaji wa takwimu na utekelezaji. Mfuko wa Kimataifa pamoja na washirika wake utatoa usaidizi katika hili. Msisite kuomba usaidizi wa kitaalam katika hili!
Kujumuisha mapendekezo ya haki za binadamu katika hatua zote za ufadhili na katika michakato ya kanuni na sera	Hii inamaanisha kwamba ushirikishaji wa kina pamoja na jamii zilizoathirika na zile ambazo hazijabaguliwa lazima ziwe miongoni mwa michakato ya ufadhili wa Mfuko wa Kimataifa, kuanzia kuandaa misaada mpaka kutekeleza, usimamizi, ufuatiliaji na kutathmini.

LENGO #4: KUHAMASISHA RASILIMALI ZAIDI

MALENGO ELEKEZI KATIKA MKAKATI	INA MAANA GANI KWETU
Kuvutia rasilimali zaidi ya kifedha na miradi kwajili ya afya kutoka vyanzo vya sasa na vyanzo vipya vya umma na binafsi	Hii inamaanisha kwamba lazima tufanye kazi pamoja ili kuhakisha kwamba Mfuko wa Kimataifa unafadhiliwa kabisa. Kwetu, hii inamaanisha kuzungumza na serikali yako, sekta binafsi pamoja na washirika wengine kuchangia Mfuko wa Kimataifa
Kusaidia nchi kutumia rasilimali zilizoko kwa ufasaha zaidi na kuongeza uhamasishaji wa kukusanya rasilimali ndani ya nchi	Hii inamaanisha tunahitaji kuwawajibisha serikali zetu katika misaada ya kiafya pamoja na bajeti za ndani. Lazima tutumie fedha za Mfuko wa Kitaifa kuendelea kuomba fedha kutoka kwa serikali zetu!
Kutekeleza na kushirikiana katika kuunda juhusi za kisoko zitakazo ongeza upatikanaji wa gharama nafuu wa dawa bora na mifumo mizuri ya kiteknolojia	Kuna sharia na kanuni ambazo zinaweza kutusaidia kupata dawa na bidhaa rahisi. Hii inamaana kwamba lazima tuchukue fursa hizo! Lazima tujielimishe kwa vitu kama haki miliki za biashara (TRIPS).
Kusaidia juhudi za kuongeza ubunifu na kuwezesha kuanzishwa na kuongeza teknolojia bora za nafuu pamoja na mbinu za utekelezaji	Hii inamaanisha tunahitaji kuendelea kuhimiza teknolojia mpya kutusaidia kuzuia magonjwa haya matatu. Inamaanisha oia kuzungumza na serikali zetu kuimasisha na kutekeleza mbinu mpya pale zinaposemakana zinakidhi majaribu pamoja na uendeshaji.

NI NINI JUKUMU LA EANNASO NA MPANGO WA KIKANDA KATIKA MKAKATI MPYA WA MFUKO WA KIMATAIFA?

- Kuimarisha mfumo wa ubia wa Mfuko wa Kimataifa: Kuhakikisha utawala bora, uwakilishi na ukaguzi kupitia mashirika yanayosaidiwa na Mfuko wa Kimataifa kama vile CCM, pamoja na kutoa usaidizi wa kitaalam kwajili ya vitu mbali mbali katika uombaji wa misaada na mchakato wa utekelezaji.
- Kujenga uwezo kupitia kuimarisha mifumo ya kijamii kwajili ya mashirika ya kiraia, makundi ya kijamii, wapokeaji wakuu, na kadhalika na kusisitiza umuhimu wa mipango ya undelevu na kutenga fedha katika miradi ya afya.
- Kusaidia ushiriki wa washiriki ya watu maalum na walioathirika na mitandao katika michakato inayohusu Mfuko wa Kimataifa
- Kuratibu na nchi, mitandao ya mashirika ya kijamii pamoja na washirika ili kuhakisha misaada kutoka kwa Mfuko wa Kimataifa inachangia kushughulikia mahitaji yote ya wanawake, vijana na watoto vizuri, kwa njia ambayo inakuza na kulinda haki za binadamu.

WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by EANNASOArusha, TanzaniaTel: +255 737 210598Email: eannaso@eannaso.org | Website: www.eannaso.org
Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: @eannaso